Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 76 No. 190 | SHAB./RAMADH. 1438 AH | MEI/JUNI 2017 | HIJRAT/IHSAN 1396 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi mlioamini, mmelazimishwa kufunga Saumu kama walivyolazimishwa wa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu. Kwa siku zilizohesabiwa. Lakini miongoni mwenu awaye mgonjwa au katika safari, basi atimize hesabu katika siku zingine. Na wale wanaoweza, watoe fidia kwa kumlisha maskini. Na atakayefanya wema kwa radhi ya nafsi yake, basi ni bora kwake; na kama mkifunga ni bora kwenu, ikiwa mnajua. (*Sura Al-Baqara 2:184-188*).

Khalifa Mtukufu awasihi Wanajumuiya

Itafuteni Taqwa kupitia saumu ya Ramadhan

Na Mwandishi wetu

Baada ya *Tashahhud, Taa'udh* na *Surat Fatihah* Hadhrat Amir-ul Muminin (atba) alisoma Aya ya 184 ya Surat Al-Baqara;

Tafsiri yake ni kama ifuatavyo:

"Enyi mlioamini! Mmelazimishwa kufunga Saumu kama waliyolazimishwa wa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu. "

Alhamdulillah (Sifa zote zinamstahikia Allah) - kwamba sisi tumewezeshwa kushuhudia tena mwezi mtukufu wa Ramadhani katika maisha yetu. Mtume (saw) mara moja aliwahi kusema kuwa 'Lau kama watu wangejua kuhusu fadhila za Ramadhani, basi *umati* wangu [Waislamu kwa ujumla] wangelitaka kwamba mwaka mzima uwe Ramadhani. Kwa kusikia hivyo, mtu mmoja alimuuliza ni zipi basi hizo fadhila za Ramadhani? Mtume (saw) alijibu: Kwa hakika pepo hupambwa tangu mwanzo hadi mwisho wa mwaka kwa ajili ya Ramadhani. Halkadhalika, katika mapokezi mengine, yaliyosimuliwa na Hazrat Abu Hurairah (ra), Mtume (saw) alisema kuwa: 'Mtu anayetekeleza ibada ya saumu ndani ya mwezi wa Ramadhan katika hali ya imani huku akijitathmini binafsi, dhambi zake zilizotangulia zinasamehewa na lau kama mngalijua ni zipi fadhila za Ramadhani, basi mngalitaka kwamba mwaka mzima uwe Ramadhani.



Msikiti wa Baitul Futuh uliopo jijini London, ndio msikiti ambao kwa kawaida Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. hutoa hotuba zake za Ijumaa na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Wakati mtu anapoongezeka katika imani, anapojifanyia tathmini binafsi, anapoangalia

Endelea uk. 3

Lord Ahmad wa Wimbledon awa Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza

Na Mwandishi wetu

Mwanajumuiya maarufu wa Uingereza anayeongoza kipindi cha '***Faith Matters***' kupitia MTA (*Muslim Television Ahmadiyya*), Lord Ahmad wa Wimbledon ameteuliwa kuwa Mwakilishi Maalum wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia katika Migogoro na Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya Jumuiya ya Madola na Umoja wa Mataifa.

Lord Ahmad ameteuliwa kushika wadhifa huo tarehe 13 Juni 2017 kufuatia uchaguzi mkuu wa Uingereza wa mwaka huu uliofanyika kwa amani na utulivu mkubwa.



Lord Ahmad wa Wimbledon

Kielimu Lord Ahmad amehitimu Shahada zake kupitia Rutlish School na London South Bank University (LSBU) pamoja na Taasisi ya Huduma za Kifedha ya Chartered.

Lord Ahmad ni mwanasiasa wa siku nyingi katika nchi ya Uingereza akikiwakilisha Chama chake cha Conservative katika nyadhifa mbalimbali tangu mwaka 2002.

Miongoni mwa nyadhifa alizowahi kuzishika ni pamoja na:

Waziri wa Anga na Biashara - Idara ya Usafiri (2016 hadi 2017), Waziri wa Kukabiliana na Misimamo Mikali - Ofisi ya Mambo ya Ndani (2015 hadi 2016), Waziri wa Usafiri - Stadi na Usalama wa Anga (2015 hadi 2016) na pia Waziri wa Jamii na Serikali za Mitaa (2014 hadi 2015).

Kuanzia 2012 hadi 2014 Lord Ahmad alikuwa kwenye orodha ya watumishi wa Serikali waliokuwa na Sifa ya kuteuliwa kuwa 'Lord' (*Government Whip and Lord in Waiting*). Kuanzia 2008 hadi

Endelea uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

KATIBA MPYA

Moja ya jamii zetu hapa Tanzania wana muarubaini wa magonjwa yote. Ugua ugonjwa wowote ukifika kwa mganga anakueleza usiwe na wasiwasi kwani ana Ndumba Yiyi - tiba ya magonjwa.

Kama hilo linawezekana katika ulimwengu wa utibabu, tunadhani hilo ni gumu sana katika ulimwengu wa siasa ambao hata dakika moja inaweza kuwa na maana kubwa.

Wanasiasa, wanaharakati wote kwa sauti moja inayoweza kusababisha gharika kilio chao ni kuwa na katiba mpya. Hivyo katiba mpya kwao ni Ndumba Yiyi - kila ugonjwa utatibiwa na dawa hiyo.

Tungeliomba kutofautiana nao. Ni sheria mama. Ni dira. Lakini sheria hiyo inatoka kwa binadamu na wao wanaotawaliwa na sheria hiyo. Lakini kuwa na katiba nzuri haikuizuia Merikani kuendelea kuwatesa na kuwanyanyasa Waamerika wenye asili ya Afrika. Inasemekana hata mwandishi wa tamko la uhuru la Merikani alikuwa na watumwa.

Hoja yetu ni kwamba inatubidi kwanza kutengeneza katiba iliyomo katika vifua vyetu. Na hapa ndipo tunapoona nafasi ya dini katika kutusaidia kutengeneza raia wema, wenye kutii sheria kwa kuelewa na kwa kumtii Mwenyezi Mungu. Katiba hata iwe nzuri kiasi gani ikianguka kwenye ardhi isiyo na rutuba itakuwa kama mbegu ambayo itachukuliwa na ndege wa angani. Watu wa dini wana wajibu mkubwa wa kulitengenezea katiba namba I ambayo ni nafsi yenye hofu ya muumbaji wa mbingu na ardhi.

Kama Mkristo anazingatia vilivyo mafundisho ya dini ya Kikristo, "Mpende jirani yako kama unavyojipenda wewe binafsi", ukikumbuka kwamba Bwana atakukataa kwani alipokuwa na njaa hukumvisha na alipokuwa hana nguo hukumvisha. Wekeni akiba zenu mbinguni kwani hapa ardhini kuna wezi. Hayo yakizingatiwa katiba mpya itakuwa na nafasi nzuri ya kutekelezwa.

Mwislamu ameambiwa kuipenda nchi kwa mahaba ya dhati ni sehemu ya imani. Hivyo kuipenda nchi, kuitumikia kwa moyo wote na bidii ni kumtumikia Mwenyezi Mungu. Mtu wa namna hii tayari anayo katiba kifuani mwake. Bila Mkristo mzuri na Mwislamu mzuri kilio chetu cha katiba mpya kinatukumbusha mshairi mmoja maarufu wa Kijerumani Goethe aliyesema "pale ambapo ndipo penye raha, nenda sasa uone ndoto zako za raha kama zitatimia".

Tumekwisha fikisha zaidi ya nusu karne toka tuwe taifa. Tuna dalili zote za kukomaa. Lazima tuwe wakweli. Lazima tutulize fikra zetu. Tutambue tatizo letu hasa ni lipi na tuende mbele. Tuliwahi kusema tatizo letu kubwa hatuna mapenzi hata kidogo na nchi yetu. Wengi tunajiona kama wakimbizi na wakati wowote tunaweza kuondoka. Hiyo ni falsafa muflisi. Lazima suala la mapenzi ya nchi liwe Ajenda maalum ya taifa. Upepo huu wa mapenzi ya nchi uvume mashuleni mwetu, wanasiasa, wafanyakazi, wakulima bila hivyo katiba yeyote ile haiwezi kutusaidia hadi tunajenga utamaduni wa kulipenda taifa letu.

Awa Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza

Kutoka uk. 1



Tariq Mahmood Ahmad sahib, maarufu kama 'Lord Ahmad wa Wimbledon' akiwa kwenye moja ya kipindi cha Faith Matters kirushwacho na Televisheni ya kimataifa ya MTA kutokea nchini Uingereza na Ghana kwa upande wa MTA Africa

2010 Lord Ahmad alikuwa Makamu Mwenyekiti (Taifa) wa Chama Chake cha Conservative.

Katika uwanja huu wa kisiasa safari yake ilianzia kuwa Diwani (Wimbledon Park) na Mjumbe wa Baraza la Madiwani katika 'London Borough of Merton' kati ya mwaka 2002 hadi 2012.

Nje ya uwanja wa kisiasa Lord Ahmad aliwahi kufanya kazi kwa muda wa miaka 20 katika Baraza la Jiji la London kwenye benki na maswala ya Fedha, ikiwa ni pamoja na Benki ya NatWest Group ambako alikuwa Meneja mwandamizi katika benki ya Ushirika na Masoko ya Fedha. Baadae aliwahi kuwa Makamu wa Rais na Mkurugenzi wa Masoko wa Alliance Bernstein na nafasi yake ya mwisho kabla ya kujiunga na shughuli za kisiasa alikuwa ni Mkurugenzi wa Mikakati na Masoko wa Taasisi ya Kifedha ya Sucden (*Sucden Financial*)

Akiwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya Jumuiya ya Madola na Umoja wa Mataifa, majukumu yake ni pamoja na kusimamia:

- Jumuiya ya Madola (kama taasisi).
- Kitengo cha Umoja wa Mataifa, cha kulinda amani, vita na Mahakama ya Kimataifa ya Makosa ya Jinai.
- Majimbo ya Nje ya Uingereza '*Overseas Territories*' (ikiwemo Falklands, Maeneo ya Sovereign Base na Gibraltar)
- Maswala ya Caribbean
- Haki za binadamu (ikiwa ni pamoja na uhuru wa dini au imani)
- Utumwa Mamboleo.
- Usalama wa Taifa: kupambana na ugaidi, kupambana na vikundi vyenye msimamo mkali na usalama Mitandaoni.
- Usalama wa Kimataifa wa sera ya Nishati.
- Shughuli zote za Mahusiano ya Nje na Jumuiya ya Madola katika 'House of Lords'

Pamoja na kuwa kwake mwanasiasa maarufu nchini Uingereza, Lord Ahmad wa Wimbledon amejipambanua wazi kwa kuwa kwake mtu wa 'Dini' akitumia vyema uhuru wake wa kuabudu bila ya kuwasumbua na kuwabughudhi wengine kwa sababu ya nafasi yake ya kisiasa.

Ameendelea kusimamia kipindi maarufu kipendwacho sana na chenye elimu nyingi cha *Faith Matters* kupitia MTA akifafanua kwa umahiri mkubwa maswala kadhaa yahusuyo Ahmadiyya na Uislamu kwa ujumla. Ni mtu ambaye amechangia kwa kiasi kikubwa katika kutoa taswira sahihi ya mafundisho ya Islam hasa katika maswala yenye utata ya Jihadi, Ugaidi na Uhuru wa Kuabudu kupitia kituo cha MTA.

Lord Ahmad ni mtu wa mfano wa kuigwa wa jinsi gani ya kutekeleza lile fundisho maarufu la Nabii Isa a.s. lisemalo: "ya Mungu mpe Mungu na ya Kaisari mpe Kaisari"

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Amsaidie sana Lord Ahmad katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku, na pia aisaidie serikali ya Uingereza na serikali zingine za mataifa mbalimbali katika kutenda haki na adili kwa wananchi wao na wanadamu kwa ujumla.

Endelea uk. 5

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Itafuteni Taqwa kupitia saumu ya Ramadhan

Kutoka uk. 1

juu ya mapungufu yake na matendo yake, anapolenga katika kutimiza haki za Allah na haki za viumbe na kujaribu kufanya matendo yake mazuri kwa kupata radhi au mapenzi ya Mwenyezi Mungu; ni katika hali hiyo tu ndipo hupata nafasi ya msamaha wa dhambi zake zilizotangulia. Hili pia ndilo lengo la kufunga katika mwezi wa Ramadhani, ambalo Mwenyezi Mungu Mtukufu amelitaja katika Qur'an takatifu.

Katika aya ambayo nimeisoma, [inasemwa kwamba] Saumu imelazimishwa kwenu katika mwezi wa Ramadhani ambao unajirudia kila mwaka ili mpate kuwa wachamungu, ikiwa na maana kwamba kila kitendo kinapaswa kufanywa kwa ajili ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Basi ni hapo tu ndipo mnaweza kufaidika na kufunga na kujiokoa nafsi zenu na mashambulio ya shetani. Iwapo mtafunga kwa usafi wa moyo, mkishika uchamungu, mtapata kuingia chini ya hifadhi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Mtume (saw) alisema: Mtu anayefunga wakati wa Ramadhani akiwa katika hali ya imani huku akijichunguza nafsi yake, dhambi zake zote zilizotangulia zitasamehewa. Ingawaje hii si imani ya kawaida. Masihi Aliyeahidiwa (as) alitufundisha kwamba hali ya imani ya kweli haiwezi kufikiwa mpaka na isipokuwa mtu amtambue Mungu. Pia alisema kuwa ni lazima tulivuke lango kubwa la kumtambua na kumuelewa Mungu kwani iwapo ufahamu wetu juu ya Mungu ni mbovu au umechanganyika na shaka au kwa namna yoyote ni dhaifu, imani yetu kamwe haiwezi kung'aa na kutoa mwanga.

Hivyo, ni kwa namna gani mtu anaweza kumtambua Mungu? Hii hutokea kupitia dhihirisho la *Rahimiyyat* (sifa ya rehema) ya Mungu; yaani kumtambua Mungu kunawezekana tu kupatikana kwa njia ya dhihirisho la sifa ya Mungu ya huruma. Anaendelea kusema kwamba wakati sifa ya Mwenyezi Mungu ya *Rahimiyyat,* neema na nguvu Zake zinapoeleweka, hizo humlinda mtu kutokana na tamaa za kimwili, kwani tamaa za kimwili huletwa na udhaifu wa imani na ukosefu wa yakini. Hivyo, inaweza kueleweka vizuri kwamba imani hii si jambo kawaida. Kwa kweli, hili ni jambo kubwa na lengo kubwa ambalo tumepewa, hilo halitimii kwa kufunga muda wa siku 30 tu, au kwa maandalizi ya mwezi wa Ramadhani, kwani haya yana umuhimu mdogo tu. Umuhimu huu unaweza tu kuongezeka wakati mafunzo yaliyopatikana mwezi huu yanaendelezwa mwaka mzima kwa juhudi zetu zote. Wakati akielezea hali ya imani na njia ya kuirekebisha, Masihi Aliyeahidiwa (as) katika sehemu moja anaandika:

"Kwa uhakika, kuna aina mbili za imani juu ya Mungu. Moja ni pungufu na inaambatana na matamshi ya mdomo tu ambayo hayana athari yoyote kwa matendo na utekelezaji. (Imani inazungumzwa lakini haionyeshwi kwenye utendaji). Aina ya pili ya imani juu ya Mungu ni ile ambayo hudhihirishwa na ushahidi wa vitendo. Anasema kwamba: "Najua kuwa watu hawa hutangaza imani yao juu ya Mungu lakini mimi naona kwamba pamoja na tamko hili, wao wamezama katika uchafu wa dunia hii na wamenajisika kwa ukungu wa dhambi."

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: "Kwa hiyo, wajibu wa kwanza wa wanadamu ni lazima kutathmini imani yao juu ya Mungu Mwenyezi. Hii ina maana kwamba ni lazima wasifanye tendo lolote ambalo linaonyesha kuwa hawana heshima na hawajali juu ya utukufu wa Mungu, wala wasipinge amri yoyote ya Mungu Mwenyezi. "Hivyo, hili ni jambo ambalo muumini anatakiwa kujichunguza mwenyewe katika mwezi huu wa Ramadhani.

Pia sasa nitaeleza nukuu juu ya jinsi gani mtu anavyoweza kupata maendeleo zaidi katika Taqwa, kama ilivyoelezwa kwetu na Masihi Aliyeahidiwa (as). Imani ya mtu hupata maendeleo wakati mtu anapofanya juhudi katika Taqwa. Wakati akiyaelekeza mawazo yetu juu ya hili, Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema: "Madhumuni ya mafundisho ya Qur'ani na Uislamu yalikuwa ni kukuza *Taqwah* [uchamungu], na jambo hili hasa haliwezi kushuhudiwa popote leo. Watu wanafunga na pia wanasali sala zao, lakini kutokana na ukweli kwamba hawana uchamungu wowote, saumu hizi na sala hizi zenyewe zinawaongoza kwenye dhambi.

"Katika zama zetu za leo, ukweli kwamba tunaona matendo ya ugaidi yakifanywa kwa jina la Uislamu, ambapo watu wasio na hatia wanauawa, haya yote yanatokea kwa sababu kuna upungufu mkubwa wa uchamungu. Siku mbili zilizopita, takriban watu mia moja waliuawa kikatili nchini Afghanistan. Je Ramadhani inaweza ikawa na faida yoyote kwa ajili ya watu kama hao [ambao wamefanya vitendo hivi]? Je, wanaweza kushiriki kwenye baraka ambazo zinatokana na neema zake? Hasha, haiwezekani, kwa sababu watu hawa wanafanya vitendo ambayo ni kinyume na amri ya Mungu Mwenyezi. Pia kwa sababu wameachana mbali na amri za Mwenyezi Mungu na wamejitenga mbali mno na uchamungu.

Sambamba na mafundisho ya Qur'an, Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema: "Hata sala bila ya taqwa ni kazi bure bali ni njia ya kuelekea jahanamu." Ni funguo ambayo humuongoza mtu kwenye jahanamu. Hivyo, ni jinsi gani Ramadhani inaweza ikawa na faida yoyote kwa wale ambao hawana taqwa yoyote?

Na kwa wale ambao hufanya mauaji kwa jina la Mungu na Mjumbe wake (saw), kamwe hawawezi kushiriki baraka za Ramadhani, bali ndio hao ambao watakabiliwa na ghadhabu ya Mungu. Hivyo, wakati tunashuhudia vitendo hivi vya kikatili na kinyama, sisi tukiwa Waahmadiya tunapaswa kutafuta toba kwa Mungu Mwenyezi kwa kusujudu mbele yake kwa wingi zaidi kuliko hapo kabla, kwani Yeye ametutenganisha na waovu hawa na Ametuwezesha kumkubali Masihi Aliyeahidiwa (as). Ni lazima kila mara tuwe makini na matendo yetu na ni lazima kujitahidi kuimarisha imani yetu.

Wakati akielezea maana halisi ya Taqwa, Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: *Taqwah* ya kweli ambayo humsafisha na humtakasa mtu na ambayo Manabii walikuja kuianzisha, imetoweka katika dunia. Je, kuna mtu yeyote ambaye ni mfano wa ***'Bila shaka Amefaulu Aliyeitakasa.'*** Usafi na utakaso ni wema mkubwa kabisa na Malaika husalimiana na mtu ambaye yu msafi. Masihi Aliyeahidiwa (as) anaendelea kusema:

'Sura ya pili [ya Kurani Tukufu] inaanza na: 'Ni mwongozo kwa wachamungu. Kusali, kufunga, kutoa *Zakat* na kadhalika vyote hukubaliwa tu wakati mtu anapokuwa mchamungu.' Na hivyo yote yaliyotajwa kabla yanaweza tu kukubaliwa wakati mtu anaposhikilia *Taqwah.* Vinginevyo hayawezi kukubaliwa kama mtu si mwenye *Taqwah.*

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: 'Katika hatua hii Mwenyezi Mungu hufuta jazba zote za mtu kufanya dhambi.' Yaani kama mtu ni mwenye *Taqwah* iliyokamilika, Mwenyezi Mungu humuondolea matamanio na hisia mbaya ambazo humshawishi mtu kuelekea kufanya makosa. Masihi Aliyeahidiwa (as) pia anasema:

'Wakati mtu awapo na haja ya mke, Yeye [Mungu] atampatia. Wakati akiwa na haja ya dawa, Yeye Atampatia. Lolote lile mtu alilo na haja nalo, Mungu Atampatia mtu huyo na Atampatia kwa njia ambazo mtu mwenyewe hawezi kuzifikiria.

Akifafanua zaidi kuhusu *Taqwah* na uthabiti, Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: "Katika hatua ya mwanzo Muislamu wa kweli anatakiwa kuonesha uvumilivu. Maswahaba wa Mtume s.a.w. walikutana na nyakati ambazo walilazimika kuishi kwa kula majani na wakati mwingine walikuwa hawana hata kipande cha mkate wa kula. Hakuna mtu anayeweza kumfaidisha mwingine isipokuwa kama imekadiriwa hivyo na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mtu anayeshika *Taqwah* milango na njia hufunguliwa kwa ajili yake. 'Yule anayemwogopa Mwenyezi Mungu - Yeye humtengenezea njia ya kuokoka na Humpa riziki kwa mahali asipopatazamia ...' Hivyo Muaminini Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa imani ya kweli.

Aya hizi zina sehemu mbili. Kwanza ni kwamba kwa wale ambao kweli wanaamini, Mwenyezi Mungu Mtukufu hufanya njia ya kuokoka kwa ajili yao na huwaruzuku kupitia njia hiyo. Sehemu ya pili ina maana kwamba Allah Mwenyezi humruzuku mtu mwenye imani ya kweli kwa njia na namna ambazo hawezi kuzitazamia. Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: 'Basi Shikilieni imani ya kweli juu ya Mwenyezi Mungu kwani mtapata kila kitu kutokana na hiyo. Lakini hiyo inahitaji uvumilivu na uimara wa kweli. Utukufu wa cheo cha Manabii ulipatikana kutokana na uimara wao na subira yao.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: 'Ni faida gani anayoweza kuipata mtu kutokana na sala na funga zisizo na uhai? (Kusali tu na kufunga kibubusa wakati wa Ramadhan hakumpatii mtu kitu chochote, bali ni ule wakati ambapo mtu anafanya hivyo kwa moyo wa dhati na kwa kudumu ndipo hapo tu anapata kila kitu). Hivyo, Mwenyezi Mungu Mtukufu anataka tuwe na uchamungu ili milango ya neema Zake iweze kuwa wazi kwa ajili yetu, na hasa katika mwezi wa Ramadhani, milango ya fadhili zake hufunguliwa zaidi juu ya wale wanaozalisha *Taqwa* ndani yao. Ili kuwa mchamungu, mtu anahitajika sio tu kuacha kufanya muovu bali pia afanye matendo mema.

Akitufafanulia juu ya hili, Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: 'Ili mtu aweze kuwa mchamungu, ni muhimu kwamba baada kuacha madhambi makubwa zaidi kama vile uzinzi, wizi, uporaji wa haki za wengine, kuonyesha kiburi, dharau na ubakhili, mtu anapaswa pia kuachana na matendo ya hali duni na kinyume chake atafute maendeleo katika kukuza khulka njema.'

Mtu anapaswa kujiepusha na tabia zote za hali ya chini na ajiendeleze katika kufikia maadili ya hali ya juu - hali hii ni ya lazima. Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema zaidi: 'Mtu anapaswa kuwatendea wengine kwa huruma, wema na kuwa na moyo safi na wa ukweli kwa Mungu. Na ni lazima mtu atafute njia za kuwatumikia wengine kwa namna inayostahili pongezi.

Mtu anapaswa kufanya matendo na kutoa huduma kwa wengine kwa namna ambayo kweli inastahili pongezi na isiyo ya kawaida katika asili yake na ni hapo tu ndipo inawezekana kwa mtu kupata kiwango cha juu cha *Taqwa.* Mtu anapaswa kumudu kutenda mazuri kwa wengine huku akionyesha moyo wa kutokuwa na ubinafsi na anapaswa kutimiza haki zinazomstahikia Mungu Mwenyezi na pia haki za binadamu wenzake kwa namna ya mfano ambayo inastahili pongezi.

Akifafanua juu ya umuhimu wa *Taqwa* na lengo la ujio wake, Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: 'Sababu hasa ya mimi kuteuliwa ni kutokana na ukweli kwamba uwanja wa *Taqwa* (uchamungu) ni mtupu. Kuna haja kubwa ya *uchamungu* badala ya kuchukua upanga ambao umetangazwa kuwa haramu. Iwapo mtashika *Taqwa,* basi dunia yote itakuja upande wenu, basi shikeni *Taqwa.* Wale ambao hunywa pombe au ambapo pombe huchukuliwa kuwa sehemu ya mila zao za kidini hawana uhusiano na *Taqwa* na wanapigana vita dhidi ya ucha Mungu.

Kwa hiyo, ikiwa Mwenyezi Mungu Mtukufu Ataisaidia Jama'at yetu kwa kuipatia watu wazuri na wenye bahati njema ambao Atawapa uwezo wa kupambana dhidi ya maovu na wao watajitahidi kupata maendeleo katika uwanja wa *Taqwa* na utakaso basi hayo yatakuwa ni mafanikio makubwa na hakuna kitu ambacho kinaweza kuwa bora zaidi kuliko hicho.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema zaidi: Kwa hiyo Jama'at yetu ni lazima iwe na hofu juu ya hili kwa sababu watakao okolewa ni wale tu wenye kiwango cha *Taqwa* ambacho Mwenyezi Mungu anataka tuwe nacho. Mwenyezi Mungu Mtukufu Ameanzisha Jumuiya hii kwa lengo la kupata *Taqwa* kwa sababu uwanja wa *Taqwa* uko mtupu kabisa. '

Baada ya Ramadhani kuna haja ya kudumu kwenye maombi yenye unyenyekevu

Na Mwandishi wetu, Dar es Salaam

Baada ya mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. alitoa hotuba ya Ijumaa akiwasihi Waahmadiyya wote duniani Kuendelea na maombi yenye unyenyekevu kwa kudumu.

Katika hotuba hiyo, baada ya *Tashahhud, Taa'udh* na *Surat Fatihah* Hadhrat Amir-ul Muminin (atba) alisema:

Ramadhani huja na baraka zisizohesabika na wale ambao wanalielewa hili wanaweza kuvuna baraka hizo. Wengi wameniandikia kwamba walikuwa na uwezo zaidi wa kufanya Nawafil pamoja na ibada za wajibu, kwamba waliweza kukamilisha usomaji wa Qur'ani Takatifu yote, kwamba waliweza kupata uzoefu wa ajabu na utamu wa kiroho, kwamba waliweza kupata uzoefu wa kukubaliwa maombi yao na kufikia yakini katika uwepo wa Mungu. Huzoor (atba) alisema: Wale ambao wameweza kujitahidi kwa namna hiyo, Mwenyezi Mungu Awasamehe mapungufu yao yoyote na Aendelee kuwabariki milele. Mwenyezi Mungu Aendelee kuinua hadhi za wale ambao waliweza kufikia vilele vya juu pamoja na wale ambao wameweza kujitahidi angalau kidogo. Hao wanapaswa pia kuomba kwa ajili yao wenyewe ili waweze kuepushwa na uvivu katika suala la kutimiza wajibu wao kwa Mwenyezi Mungu na kwa viumbe wa Mwenyezi Mungu. Wakati Mwenyezi Mungu Anaposema kwamba Anakuja karibu na mtumishi wake anapomuomba, habari hii si kwa ajili ya mwezi wa Ramadhani tu, badala yake Anasema kwamba daima Anayajibu maombi ya mtu mwenye shida pale anapomwomba. Mwenyezi Mungu hakujifunga kuwapatia waja ukaribu Wake katika mwezi wa Ramadhani tu. Mwezi huu umekuwa maalum ili kuvuta hisia zetu tu. Tangazo "***Mimi nipo karibu***" ni kwa ajili ya muda wote.

Akitukumbusha wajibu wetu juu ya Sala, Mtukufu Mtume s.a.w. anasema kwamba Mwenyezi Mungu anakuwa karibu zaidi na mtumishi wake katika sehemu ya katikati ya usiku, na hivyo ikiwezekana mtu anapaswa kumkumbuka Mwenyezi Mungu katika muda huo. Huzoor (atba) alisema: Iwapo mmezalisha tabia ya kusali Nawafil katika mwezi wa Ramadhani, basi mnapaswa kujaribu kuidumisha tabia hiyo kwa kudumu. Kama sisi tutadhamiria kiukweli, tunaweza daima kuendelea kunufaika na ukaribu wa Mwenyezi Mungu . Wakati Mwenyezi Mungu anapokuwa karibu na mtu, basi mtu huwa chini ya hifadhi Yake.

Yule anayemkumbuka Mwenyezi Mungu ni kama mtu aliye hai, na ambaye hamkumbuki Mwenyezi Mungu ni kama yule aliyekufa. Mtu kumkumbuka Mwenyezi Mungu kwa muda wa siku chache tu (na kisha akajisahau) kunamfanya kuwa mtu aliyekufa kiroho. Kama tunataka kuwa miongoni mwa walio hai kiukweli, tunapaswa kumkumbuka Mwenyezi Mungu katika miezi 11 iliyobaki pia. Baada ya kuwa chini ya ulinzi wa Mwenyezi Mungu katika mwezi wa Ramadhani, tunapaswa kutumia njia zote na kwa kudumu kujiweka sisi wenyewe chini ya ulinzi Wake.

Huzoor (atba) akasema: Mola wetu ni mkamilifu na kabisa si mhitaji wa yeyote, Yeye hamjali mtu isipokuwa awe anamuomba kwa bidii na mara kwa mara. Hivyo ni muhimu kwamba tuhisi huruma ya kweli wakati tunapoomba kwa ajili ya mtu yeyote. Kama vile ambavyo sisi huomba kwa bidii kwa ajili yetu wenyewe, kwa namna hiyo hiyo tunapaswa kuomba kwa ajili Jama'at, tunapaswa kuomba kwa ajili ya umma wa Kiislamu, na pia tunapaswa kuomba kwa ajili ya nchi zetu husika. Tunapaswa pia kuomba kwamba Mwenyezi Mungu Aziondoe hatari ambazo zimeizunguka dunia kote leo. Tunapaswa pia kutokuwasahau hata maadui zetu katika maombi yetu. Kila uwigo wa maombi unavyokuwa mpana, ndivyo hivyo faida kubwa zaidi inavyopatikana kwa mtu ambaye anaomba. Na kila mtu anapokuwa bahili katika maombi yake, ndivyo hivyo hivyo anavyojiweka mbali zaidi na Mungu.

Huzoor (atba) akasema: Katika maombi yetu ya kila siku tunapaswa kuiombea Jama'at pia. Kila mmoja anafahamu vyema juu ya hali ilivyo mbaya nchini Pakistan. Mara kwa mara kuna kesi za kisheria zinazofunguliwa dhidi ya Wanajama'at au Waahmadiya wanasumbuliwa kwa njia moja au nyingine na Mamula au na viongozi wa serikali. Mwenyezi Mungu Amlinde kila Muahmadiyya dhidi ya shari zao. Wakati mwingine serikali hufanya mambo fulani ili kujenga sheria na taratibu ambazo huwasaidia kutekeleza sheria kali ili kusaidia kuimarisha serikali zao. Vitendo kama hivyo vilifanywa na serikali zilizopita pia. Kwa hiyo, maombi maalum yanahitajika. Waahmadiyya nchini Pakistan wanapaswa hasa kujiombea wao wenyewe. Sisi daima hatujawahipo kujichukulia sheria mikononi mwetu, wala hatujataka kulipiza kisasi, na kamwe hatutofanya hivyo katika siku zijazo. Silaha yetu ni maombi, na ni silaha hiyo tu ambayo tutaitumia daima. Mwenyezi Mungu daima Ameendelea kutulinda dhidi ya mipango yao miovu na Inshallah Ataendelea kufanya hivyo na Jama'at itakuwa na maendeleo zaidi kuliko hapo kabla.

Huzoor (atba) alisema: Matendo yanayofanana (na hayo ya Pakistan) yanaendelea pia nchini Algeria, lakini Waahmadiya wote ukiondoa wachache sana wamebaki imara katika imani yao. Muahmadiyya mmoja aliandika kwamba ingawaje Jama'at iliimarishwa hapa miaka kumi tu iliyopita, historia yao ya kujitolea inaenda miaka mingi nyuma. Serikali pia inashangaa kwamba imekuwaje watu hawa hawarudi nyuma katika imani yao wala hawaonyesha makabiliano yoyote hasi. Hii ni kwa sababu wanayo silaha ya maombi na wanaamini kwamba muda wao wa dhiki utafikia mwisho na Mwenyezi Mungu Atayasikiliza maombi yao. Mbele ya Mwenyezi Mungu, nguvu za mamlaka za kidunia hazina thamani yoyote. Mitihani huja na dhabihu hubidi kufanywa, lakini ushindi wa mwisho ni wa wale wanaobaki pamoja na Mwenyezi Mungu. Historia ya Jama'at inaonyesha kwamba katika kila tukio Mwenyezi Mungu Alibaki kuwa pamoja na Jama'at na Aliilinda, na adui daima alibaki akiwa amechanganyikiwa.

Huzoor (atba) alisema: Wale ambao wanadhani kwamba hawakabiliwi na hatari yoyote ya moja kwa moja na hivyo wanakuwa wazembe katika sala zao na maombi yao wanapaswa kukumbuka kwamba majaribio hayo yanaweza kuwafikia wao pia. Hivyo kabla hilo halijatokea kwao, wanapaswa kurejesha uzingativu wao kwenye maombi. Hata kama ninyi mnaishi katika utulivu na usalama, mnapaswa kuwaombea ndugu zenu Waahmadiyya kwa moyo wa huzuni ili kwamba Mwenyezi Mungu Apate kuwasaidia katika dhiki zao. Wakati mtu anapoomba kwa ajili ya wengine, matatizo binafsi ya mtu huyo pia huondolewa.

Huzoor (atba) alisema: Wale wanaoishi katika nchi za Magharibi wanapaswa kutokujifikiria kwamba wako salama, kwa sababu Waahmadiyya pia watapata athari kutokana na kuongezeka kwa hisia zilizo dhidi ya Waislamu. Ingawaje tunasema kwamba sisi ni Waislamu tupendao amani, lakini mtu yeyote anaweza kutushambulia kwa upofu. Matukio kama hayo yameanza kutokea ambapo wale wanaopinga Waislamu na wale wanaotukuza utaifa wameanza kufanya matendo yaliyo dhidi ya Waislamu.

Huzoor (atba) alisema: Hali dunia nzima ni kana kwamba inavutia ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Mataifa yenye nguvu yanajaribu kusababisha mipasuko kati ya mataifa ya Kiislamu, na hali hii inaweza kuzirejesha nchi hizi nyuma kwa miongo kadhaa. Marekani ina malengo ya hatari. Migogoro imeanzishwa katika Syria ambayo inaweza kusababisha Iran kutuma majeshi yake huko, na kama hilo litokezee basi litaipatia Amerika na Israel sababu ya kuwasha zaidi moto wa uhasama wao dhidi ya Uislamu. Mataifa makubwa kwa njia za ujanja sana yajaribu kuzidhoofisha nchi za Kiislamu. Ingawaje migongano hii haitobaki tu katika eneo fulani, Urusi pia inaweza kujiingiza na hapo hali inaweza kubadilika na kuwa vita ya dunia.

Nchi za Kiislamu zitarudi nyuma miongo kadhaa. Mvutano kati ya Marekani na Korea pia unazidi kukua na wachambuzi wanasema kwamba matumizi ya hata silaha ndogo tu kwa upande wa Amerika yanaweza kuzidisha hatari ya vita ya kutisha katika eneo hilo. Huzoor (atba) alisema kuwa uvumbuzi mpya unaweza pia kuwa njia ya uharibifu, kama vile mashambulizi ya kimtandao hasa kama yatatumika katika kuzalisha silaha za maangamizi.

Huzoor (atba) alisema: Dunia inajitengenezea yenyewe njia za maangamizi yake.

Hazur (atba) amesema: Viongozi wengi wa nchi za Kiislamu tayari wameisha waudhi raia wao wenyewe kwa kufanya mauaji dhidi yao, na wanaweza kufanya mauaji mkubwa zaidi ili kulinda utawala wao, lakini hilo sio suluhisho. Suluhisho ni lili tu lililoelezwa na Mtume Mtukufu (saw), ambalo ni kumkubali Mahdi Aliyeahidiwa. Sisi tunayo bahati kwamba, kwa kuzingatia amri ya Mtume Mtukufu (saw), tumemkubali Masihi Aliyeahidiwa (as). Ni Waahmadiyya pekee wanaoweza kuiokoa dunia kwa maombi yao ya dhati. Kila Muahmadiyya ni lazima ahisi mateso ya watu wote wa dunia na awaombee. Majanga yanaikumba dunia kwa haraka sana. Wakati tunaeneza ujumbe kwamba wokovu upo tu kwa kuja chini ya ulinzi wa Masihi Aliyeahidiwa (as), ni lazima pia tuombe kwa ari kwamba Mungu Aipe dunia akili na Aikoe katika maangamizi.

Ninamuomba Mwenyezi Mungu Atuwezeshe kuileta dunia chini ya bendera ya Mtume mtukufu (saw). Ninaomba sisi tutumie njia zote na tupaishe maombi yetu kileleni ili kulifanikisha hili. Baada ya Ramadhan pia tuendelee kuja karibu zaidi ya Mwenyezi Mungu kwa ibada na maombi. Ninamuomba Allah mwishowe Atupatie ushindi. Amīn.

بسم الله الرحمن الرحيم

JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA TANZANIA - KALENDA YA MATUKIO KWA MWAKA 2017/2018

MWEZI	MWAKA	TAREHE	TUKIO
JULAI	2017	01 – 10	Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa – Dar es Salaam.
		10 – 15	Siku maalum za kukutana na viongozi wa serikali/waandishi wa habari sehemu walipo kwa lengo la kuleta uhusiano nzuri.
		17 – 24	Siku maalum za makusanyo ya michango ya Waqf-e-Jadid na Tahrik Jadid
		28 – 30	**Jalsa Salana Uingereza**
AGOSTI	2017	1 – 8	Maonyesho ya Kilimo kitaifa - Mikoa husika
SEPTEMBA	2017	1 – 10	Siku maalum za maonyesho ya vitabu katika Mikoa husika.
		02	**Eid Ul Adhha***
		07 – 14	Wiki maalum ya kuchanga mchango wa mkutano wa mwaka (Jalsa Salana)
		19 – 20	Uendeshaji wa semina za Tabligh katika kila tawi.
		29-30	**Jalsa Salana Tanzania**
OKTOBA	2017	1	**Jalsa Salana Tanzania**
		24	Siku ya mwisho ya kupokea ripoti za makusanyo ya Tahrik Jadid 2016/17
NOVEMBA	2017	4-5	**Siku maalum za mahubiri nchi nzima.** Mahubiri yafanyike, viongozi wote wa Matawi ni lazima washiriki, ripoti itumwe Makao Makuu.
		15 – 29	Ahadi za Tahrik-e-Jadid kwa mwaka mpya (Novemba 2017 / Oktoba 2018)
		19	**Siku ya waanzilishi wa dini.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii hii).
		26	Mitihani kutoka kitabu cha: **Mgogoro wa Dunia na Njia Kwenye Amani (1/3)**
DISEMBA	2017	01 – 15	Siku maalum za kukusanya malimbikizo ya Waqf-e-Jadid.
		16 – 17	Ijtimaa ya Ansarullah Kitaifa - Dar es Salaam
		24 – 31	Siku maalum za Tarbiyyat Kitaifa. (Msukumo uwekwe zaidi kwa Waahmadiyya wapya).
		24	**Siku ya Seeratu Nabii.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii).
JANUARI	2018	06 – 20	Ahadi mpya za Waqf-e-Jadid kwa mwaka 2018.
		21	Mitihani kutoka Kitabu cha: **Mgogoro wa Dunia na Njia Kwenye Amani (1/3)**
		24 – 31	Siku maalum za makusanyo ya mchango wa kawaida.
FEBRUARI	2018	01 – 06	Siku maalum za kuwaalika wageni kwa mazungumzo katika Jamaat zote. Taarifa zitumwe Makao Makuu.
		20	**Siku ya Mwana Aliyeahidiwa.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii).
		24 – 25	Siku maalum za kuwatembelea wagonjwa, mahospitalini na majumbani. Pia kuwatembelea mayatima, walemavu, na vikongwe (washiriki, Ansar, Khuddam na Lajna).
MACHI	2018	01 – 09	Siku maalum za kufanya vikao vya kujadiliana ajenda za Shura ya 2018 na kuchagua wajumbe.
		10 – 11	Mahubiri Maalum kwa kila tawi. (Viongozi wote ni lazima washiriki).
		18	Mahubiri ya tarehe 12 – 13 yatolewe maelezo yake mbele ya Wanajumuiya wote.
		23	**Siku ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii).
		31	Siku ya mwisho ya kutuma dondoo za Mushawara kutoka matawini kwa ajili ya Shura ya mwaka 2018.
APRILI	2018	08	Mitihani kutoka kitabu cha: **Mgogoro wa Dunia na Njia Kwenye Amani (1/3)**
		08 – 15	Siku maalum za kukusanya malimbikizo ya mchango wa Tahrik Jadid na Waqfe Jadid.
		28 - 29	**Shura ya Kitaifa Dar es Salaam – mwaka 2018.**
MEI	2018	09 –16	Siku maalum za kukusanya malimbikizo ya michango. (Hasa mchango wa kawaida).
		13	Wajumbe wa Shura wayaeleze matawi yao maazimio ya Shura - 2018
		17	**Kuanza kwa mfungo wa mwezi wa Ramadhan**
		27	**Siku ya Ukhalifa.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii hii).
JUNI	2018	01 – 15	Siku maalum za kuhakikisha kwamba kila Mwanajumuiya amekamilisha Bajeti ya michango yake hasa wa kawaida/Wasia sawa na kiwango cha kila mwezi. Juhudi maalum zifanywe.
		22-24	**Ijtimaa ya Khuddamul Ahmadiyya Kitaifa.**
		29-30	**Ijtimaa na Shura ya Lajna Imaillah Kitaifa.**

***Zingatia: Saumu ya Ramadhani, na Sikukuu zote mbili zinategemea kuandama kwa mwezi.**

Bustani ya Washairi

KHUDDAMUL AHMADIYYA.

1. Bismillah auni, ya ilah ya manani
Wachumba wako kundini, wenye nzuri tabia
Wanaifahamu dini, sio suni kadiria
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

2. Tuoe walokundini, vijana nawausia
Kundini kuna madini, usunini utalia
Tena visu vya mpini, Hata huwezi umia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

3. Nyi jipalaganyaneni, kwa kufuata parokia
Tafadhalini wahuni, tutamuasi Jalia
Zungukeni majumbani, tapata pa kuanzia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

4. Warefu wapo kundini, vijana chakalikia
Wenye rangi za madini, na sauti za kulia
Kitembea sakafuni, ana anza na wakulia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

5. Wanaisoma Qurani, na Sala kujisalia
Chukua uweke ndani, usije ukajutia
Uwe wewe awe nani, naweza kujililia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

6. Jikoni wako makini, mchuzi kukupikia
Kuyakaanga maini, na wali kuupalia
Na samaki saladini, kwa nazi kukuungia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

7. Si kwa usafi wa ndani, sebule kupangilia
Wanaanzia bafuni, jikoni kumalizia
Wako vizuri chumbani, Mimi ndio nakwambia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

8. Kwa majuba magauni, na marashi kunukia
Kuwakirimu wageni, zawadi kuwapatia
Wanaheshimu ukweni, na simu kuwapigia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

9. Wanja mwingi machoni, na udi wana nukia
Hereni masikioni, Shungi zinaning'inia
Wanayo haya machoni, chini wanaangalia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

10. Hawayasemi ya ndani, siku wakijikalia
Yanaishia chumbani, hata wakijililia
Hayafiki sebuleni, watoto watasikia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

11. Ukimuomba manani, Sala kwikwi na kulia
Utawaona ndotoni, mlimbwende takujia
Usijifanye huoni, na acha kulia lia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

12. Vijana angalieni, tena mtakuja lia
Nawaomba wajameni, huku wanawalilia
Tuoeni huku ndani, tupanue jumuia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

13. Nendeni hata Manyoni, warembo kujipatia
Itangulizeni dini, Mola atajaalia
Waoeni wa kundini, huko nje mtajutia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

14. Msisahau tambani, mara moja kupitia
Kuna watu wa kundini, unaweza jipatia
Wanaifahamu dini, kitonga kujitolea
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

15. Piteni na magomeni, Kagera kuulizia
Watu wake ni makini, ndoa wanaililia
Tajipatia kidani, mtani tatutambia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

16. Mnachelewa kwa nini, kichwa changu naumia
Muko mahusianoni, kutwa unajipigia
Mnapata ahuweni, ndo mana mmetulia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

17. Nendeni hata dutumi, watu wanawalilia
Wanataka ahuweni, ndoa kujifagilia
Pia kuna Qadiani, kitonga sio India
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

18. Mwezi wa Ramadhani, saumu najifungia
Kulikuwa na tafrani, wapi pa kufuturia
Ninafuturu nyumbani, Hawa ananipikia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

19. Tuwaoe wa kundini, na tusiwapige pia
Tutalipwa na Manani, thawabu tajipatia
Kuna visu vya mipini, utakuja niambia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

20. Usijivishe mawani, Kingugi hujapitia
Kujifanya hauoni, kinanda kinacholia
Tubakie jamatini, raha tutajipatia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

21. Da! Morogoro kunani, mmoja amebakia
Eneo msikitini, shungi anajivalia
Kiongozi wa tawini, Jikoni anapatia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

22. Vipi kimanga tawini, vimwali wamejazia
Kama hauko makini, poa utachukulia
Sisahau kigamboni, kwa dini amekulia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

23. Mikumi ya Magomeni, jaribuni kupitia
Kuna kinanda makini, aibu kajazilia
Gongolamoto kunani, kimya anajikalia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

24. Al Islam ddin, katukumbusha Jalia
Tujibakize kundini, ndipo pa kukimbilia
Kijifanya majinuni, mwishowe tajililia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

25. Nimefikia mwishoni, kazi kwako fatilia
Nimeshakupa ramani, hapana kulialia
Usiwazie ndotoni, pita kwenye familia
Nawaasa nawaomba, yatawakuta mazito

Litaendelea;

Abdallah S. Kalindima
(K-mtoto)
kmtoto1@gmail.com

KARNE YA UKHALIFA, SHANI YA AHMADIYYA

1. Kwako ninakimbilia, Ewe mwenye kila sifa,
Nakuomba nipokea, ona nilivyo dhaifa,
Niweze kuisifia, karne ya Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

2. Shani ya Ahmadiyya, karne ya Ukhalifa,
Umri miaka mia, imara bila ya nyufa,
Haijapata tokea, kwa umma wa Mustafa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

3. Zama zilipowadia, za yalotajwa maafa,
Wengi walipodhania, Islam ni ulofa,
Mola Akakadiria, kukuza yake sharafa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

4. Ndipo akamteua, Ghulamu alo nadhifa,
Elimu kamshushia, akampa na wadhifa,
Apate ongoza njia, kusherehesha suhufa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

5. Mirza akanadia, kuyaita mataifa,
Mimi ndiye Masihia, njooni mupange safa,
Akazidi shadidia, Yesu ameshatawafa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

6. Kuaga kwake dunia, hakukuwa kwa kifafa,
Aliandika wasia, wenye njema taarifa,
Mola ameniambia, musubiri ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

7. Wale walotegemea, Silsila itakufa,
Mara wakashuhudia, nguvu za Mola Raufa,
Kwenye nyayo za Nabia, ukaota Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

8. Nuruddin awalia, akavishwa ukhalifa,
Akaivusha Jamia, kwenye kubwa taklifa,
Nuhusi ikakimbia, kuupisha Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

9. Bashirudin thania, kaupamba Ukhalifa,
Kaijenga Jumuia, kwa makubwa maarifa,
Nidhamu katuwachia, ili tubaki Hanifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

10. Nasir alotulia, mhifadhi msahafa,
Nafasi ya thalathia, kauhami ukhalifa,
Bunge la kijahilia, likagubikwa kashifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

11. Twahir arbaia, kaukuza Ukhalifa,
Ikashamiri Jamia, mikoa hadi tarafa,
Wapinzani kina zia, wakadondoshwa ghorofa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

12. Masroor Khamsia, tuliyenaye Khalifa,
Ayyadahu Naswria, mambo yawe ashrafa,
Tuzidi itumikia, dini ya Mola Latifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

13. Leo twasherekea, karne ya Ukhalifa,
Matunda twajivunia, Jannati Alfaafa,
Sote tunashukuria, neema ni Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

14. Jamaat Ahmadiyya, hoja yetu ukhalifa,
Nyoyo zitele khushua, roho zetu ni Arafa,
Ziko safi zetu nia, watulinda Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

15. Jamaat Ahmadiyya, ngome yetu Ukhalifa,
Wenyewe twajichangia, milioni za sarafa,
Mola Ametuokoa, watutosha Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

16. Dini twaipigania, Jemedari Ukhalifa,
Idara za Tarbia, Ishaat na tasnifa,
Ewe mtafuta njia, njoo kwenye Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

17. Ummati Muhammadia, uzima ni Ukhalifa,
Wapi mtakimbilia, muipate takhfifa,
Ndwele mnazougua, dozi yake ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

18. Dini ya Islamia, umoja ni Ukhalifa,
Kugombania ulua, na vipando vya masofa,
Fujo zitaendelea, kwa kukosa ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

19. Aloahidi Jalia, kuuleta Ukhalifa,
Kwa waliominia, na vitendo insafa,
Kama wetu ni kuzua, anzisheni Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

20. Karne tunaishia, zindabad Ukhalifa,
Sisi na wetu dhuria, tuandame ukhalifa,
Ije mia kisha mia, upevuke Ukhalifa,
Karne ya Ukhalifa, Shani ya Ahmadiyya.

Safari ya Sialkot ya Seyidna Ahmad a.s. 1904

Na Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, Rabwah, Pakistan.

Seyidna Ahmad a.s. Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya aliponuia kwenda Sialkot, basi tarehe 27 Oktoba 1904 saa kumi asubuhi Hudhur a.s. alitoka Qadian, ahli zake pia walikuwa pamoja. Kutoka Batala stesheni behewa moja ya daraja ya pili na behewa moja ya wastan zilipangwa. Wakati wa kufika Amritsar wanajumuiya wa pale waliwaletea chakula, Hudhur a.s. alichokubali. Garimoshi lilipofika Lahore watu walijumuika kwenye stesheni kiasi hiki kwamba ilikuwa vigumu kwa maafisa wa reli na polisi kuwapanga. Kwenye stesheni ya Wazirabad pia watu walikuwa wengi kiasi hiki kwamba ikawa vigumu kwa wafanyakazi wa reli kuondoa behewa yake iliyopangwa kwa kuunganisha na gari la Sialkot. Wanajumuiya wa Wazirabad pia waliwapatia Hudhur na wenzake soda na sharbati ya limau.

Kufika Sialkot:

Ingawa gari lilifika Sialkot stesheni baada ya magharibi, hata hivyo stesheni ilijaa sana mno kwa wenye shauku ya kumwona. Hudhur a.s. na wenzake walipopanda magari kwa kwenda mahali pa kukaa, nje mpaka mwisho wa kuona walikuwa watu tu. Mamia ya watu walikimbia pamoja na gari lake. Agha Muhammad Bakir Khan, Hakimu wa heshima alitembea mbele ya gari la Hudhur a.s. kwa kupanga watu. Njiani kwa kuweka mwanga mbele ya gari la Hudhur a.s. mioto iliwashwa. Ilipangwa kukaa kwa Hudhur a.s. katika nyumba ya Hadhrat Hakim Hisamuddin.

Karamu ya wanajumuiya wa Sialkot:

Kwa vile nyumba ya Hadhrat Hakim haikutosha kwa kukaa kwa ndugu wote, kwa hiyo wanajumuiya wengi wa maeneo yale waliacha nyumba zao kwa wageni kwa njia hii kwamba mitaa yote ikawa kama nyumba moja. Katika kila chumba maji na mwanga wa kutosha ulipangwa. Jumuiya ilipanga maduka ya waganga wa mji kwa kupata dawa bure. Mpango wa chakula ulikuwa hivi kwamba wageni kutoka Qadian walikuwa wakipewa chakula makazini mwao na wageni wengine waliokuja kutoka wilaya za Sialkot, Gujaranwala, Lahore, Jehlum, Gujrat na kadhalika walikuwa



Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, aliyewahi kuwa Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahamdiyya nchini Tanzania kwenye miaka ya 1999 - 2001

wakipewa chakula katika uani moja kubwa.

Ukaribisho:

Nilisahau kutaja kwamba wakati wa ujio wa Hudhur a.s. katika Sialikot, Jumuiya iligawa ukaribisho uliochapwa ambamo ziliandikwa beti hizi mbili:

Ujio wako ni raha kwetu,
kukutaja ni nyimbo ya furaha yetu.

Ee Mola, weka kivuli chako juu ya moyo wetu mpendwa,
Ee Khidhiri wetu, Mahdi wetu, Isa wetu na Mirza wetu.

Hotuba ya Hudhur a.s. baada ya sala ya Ijuma:

Siku ya pili tarehe 28 Oktoba ilikuwa Ijumaa. Sala ya Ijumaa katika Msikiti wa Hadhrat Hakim Hisamuddin, Hadhrat Maulawii Abdul Karim alisalisha na katika hotuba ya Ijumaa alieleza maelezo ya Sura Al-Jumu'a. Baada ya sala watu wengi walifanya baiati, Kwa vile idadi ya wafanyao baiati ilikuwa kubwa sana, kwa hiyo vilemba 12 vilisambazwa kwa jeha mbalimabli, watu wakivishika walirudia ahadi ya baiati. Baada ya baiati Hudhur a.s. alitoa hotuba fupi ambamo alieleza uhakika wa baiati na alisisitiza kutanguliza dini juu ya dunia. Hotuba hiyo ilichapwa katika magazeti ya Jumuiya. Baada ya sala ya Ijumaa kwa kukaa na watu kwa muda mrefu hali ya Hudhur a.s. iliathirika vibaya, kwa hiyo siku mbili zijazo yaani 29 na 30 Oktoba Hudhur a.s. hakuweza kuja nje. Tarehe 31 Oktoba 1904 Hudhur a.s. alidhihirisha nia yake ya kurudi, kwani wageni walijumuika zaidi sana ya mategemeo na Hudhur a.s. alihofia sana kwamba isije Jumuiya ya Sialkot itaabike kwa kuwalisha wageni. Hadhrat Hakim alipojua jambo hilo basi mara alimfikia Hudhur a.s. na akitaja akiba ya vyakula vyake alimwomba Hudhur a.s. kuahirisha nia yake. Hudhur a.s. alimjali sana Bwana Hakim kwani alikuwa na mahusiano naye tangu siku za kuajiriwa katika Sialkot. Kwa hiyo aliahirisha nia yake ya kurudi.

Pendekezo la hotuba ya hadharani:

Iliamuliwa kwamba katika Sialkot hadhara moja ipangwe. Basi kwa lengo hilo baada ya kupanga tarehe 2 Novemba 1904 ilitangazwa kwa matangazo na Hudhur a.s. alishughulikia kutayarisha hotuba. Kwa hiyo tarehe 31 Oktoba 1904 pia Hudhur a.s. hakuweza kuja nje. Idadi ya wapendao kumwona iliendelea kuzidi. Kuona hali hiyo Hudhur a.s. aliombwa kwamba akae kwa muda fulani katika dirisha la ghorofa ili watu waweze kumwona kutoka mitaani. Hudhur a.s. akaja dirishani lakini kwa kujumuika maelfu ya watu, alihofia kwamba isije mzee, mtoto au dhaifu yeyote akanyagwe na halaiki, akisimama kwa dakika moja tu alirudi.

Alikuwa na ufululizo wa kalamu kiasi hiki kwamba Baadhi ya wakati aliandika kitabu cha mamia ya kurasa katika siku chache. Hotuba ya Sialkot iliyo hotuba ya juu sana, Hudhur a.s. alianza kuiandika baada ya adhuhuri ya 31 Oktoba na tarehe mosi Novemba ilichapwa tayari. Hotuba ilikuwa juu ya "Islam" iliyopangwa kusomwa katika nyumba ya wageni ya Maharaja Jammu tarehe 2 Novemba 1904 saa moja asubuhi. Mkutano ulifanyika uani mwa nyumba ya wageni ya Maharaja Jammu ambamo ilipangwa mikeka na mahema kwa uwingi.

Kwa vile Hadhrat Maulawii Abdul Karim akija kabla ya Hudhur a.s. alitoa hotuba mbili katika mji hadharani na matangazo pia yalisambazwa kwa uwingi, kwa hiyo masheikh wapinzani kwa kuzuia watu kufika mkutanoni siku hiyo asubuhi saa kumi na mbili na nusu walianza kutoa hotuba za kukataza katika sehemu mbali mbali mjini. Hata hivyo watu walijumuika kusikiliza hotuba ya Hudhur a.s. wengi kiasi hiki kwamba ikawa vigumu kupanga kuwakalisha.

Kwenda mkutanoni:

Hudhur a.s. alienda mkutanoni kwa sura ya msafara, kwa magari 15-16. Hadhrat Maulawii Abdul Karim alikaa na Hudhur a.s. na kwa gari la Hudhur a.s. kwa kupanga njia Sardar Muhammad Yusuf Khan, Hakimu wa mji alikuwa akitembea. Pande zote mbili halaiki ilijumuika kwa uwingi kiasi hiki kwamba kwa taabu sana njia ilipatikana kupitia magari. Njiani majukwaa ya masheikh wapinzani pia yalionekana. Masheikh walizuia watu kwenda mkutanoni kwa kupaza sana sauti lakini matokeo yake yalikuwa haya kwamba watu waliojua tayari mahali pa mkutano walielekea huko lakini ambao hawakujua pia kwa hotuba za masheikh walipajua na walienda mbio mkutanoni. Mungu Akitaka adui pia anasababisha heri.

Hotuba ya uraisi ya Hadhrat Maulana Nuruddin r.a.:

Hudhur a.s. alipofika mkutanoni, aliona kwamba maelfu ya watu wa kila dini na kabila wameshajumuika. Waheshimiwa wa mji walikuwa na rai hii kwamba mpaka leo katika Sialkot watu wengi kiasi hiki hawajaonekana katika hotuba ya mtu yeyote. Kwenye jukwaa pamoja na Hudhur a.s. walikaa Hadhrat Maulawii Abdul Karim na wazee wengine. Baadhi ya waheshimiwa wa mji pia walikaa hapo. Kwa maoni ya Mian Fadhl Husain Barrister na kwa kuungwa mkono na wahudhuriao Hadhrat Maulana Hakim Nuruddin akawa mwenyekiti wa mkutano. Katika hotuba yake nzuri na fupi aliwaambia wahudhuriao kwamba watu ambao kutosikiliza mambo yao watu watalazimika kusema siku ya kiyama kwamba: Laiti tulikuwa tunasikia na kutafakari kwa kutumia akili basi leo tusingepata taabu. Mfano wa watu hao mtasikiliza hotuba yake saa hii. Kwa hiyo sikilizeni kwa makini na muifuate.

Hotuba ya Hudhur a.s.:

Baada yake alimwomba Hadhrat Maulawii Abdul Karim kusoma hotuba ya Hudhur a.s. Hadhrat Maulawii Abdul Karim mwanzoni alisoma kwa sauti nzuri na kubwa fungu la mwisho la Sura Al-Hashr kisha alianza kusoma hotuba ya Hudhur a.s. kwa njia safi sana ya kuvutia. Kueleza mandhari ya wakati ule ni nje ya uwezo wetu. Watu kwa makini sana walisikiliza hotuba ya Hudhur a.s. hata watu wengi walisimama juani pia.

Sifa kubwa ya hotuba hiyo ilikuwa hii kwamba akieleza madai yake mara ya kwanza kabisa alijitaja kama mithili wa Krishna pia. Kisha akiwahutubia Mabaniani na Maariya alisema kwamba nawasihini hivi kwa kuwa Krishna kwamba kuamini ya kuwa mata na roho ni tangu azali na za kudumu pamoja na Mwenyezi Mungu ni itikadi batili na iliyojaa ushirikina. Kwa hiyo iacheni itikadi hiyo. Vile vile alisema kwamba itikadi ya tanasukh pia ni batili na Niyoga ni kitendo kichafu kiasi hiki kwamba ni aibu kuieleza pia. Baada ya hotuba kumalizika wakati wa kurudi makazini kwa wenzake katika gari lililofungwa, njiani wapinzani walianza kupiga mawe garini lakini kwa fadhili na rehema ya Mwenyezi Mungu Hudhur a.s. alifika makazini kwa usalama. Kwa kuona fitina za wapinzani, Inspekta polisi Mzungu wakati ule aliyekuwa kazini, aliwaambia masheikh; "twashangaa kwamba kwa nini mnampinga mtu huyu, twapaswa sisi Wakristo au Mabaniani kumpinga kwani anapinga dini yetu. Anathibitisha Islam kuwa dini ya kweli, anaangamiza dini yetu, mnampinga bure."

Uwingi wa wafanyao baiati:

Tarehe 3 Novemba 1904 ilipangwa kwa kurudi kwa

Endelea uk. 9

Mbashiri wa kwanza Mzalendo wa kujitolea Afariki

Na Al-Ustadh Khamisi Sultan S. Wamwera – Dar es Salaam



Al-Ustadh Khamisi Sultan S. Wamwera



Al Marhuum Sheikh Swaleh Mbaruku Kapilima

Kutoka toleo lililopita

Mnamo tarehe 05 mwezi wa 8, mwaka 1958 palikuwa na mjadala kabambe kati ya Sheikh Swaleh na Maulamaa wa Kisuni kuhusu Talakini. Matokeo ya mjadala Maulamaa wa Kissuni waliambulia patupu. Watu waliofatilia mjadala huo pamwe na wale wanafunzi wake, wengi wao waliafikiana na Sheikh Swaleh. Maulamaa hao kwa kushindwa hoja waliwaambia watu kwamba wasimfuate Sheikh Swaleh, huyo ni Kadiani si Mwislam. Ndipo Sheikh Swaleh akaanza kueleza maana ya Khattamn Nabibiyyin, kuendelea neema ya Utume na kifo cha Nabii Isa (as). Wenye bahati masikio yao yakafunguka, ukweli kuukubali.

TAWI LA JUMUIYYA LAANZISHWA.

Kama Rufiji, wanafunzi wa Sheikh Swaleh na wenyeji wa kijiji cha Njinjo waligawanyika. Baadhi walikubaliana na Sheikh na wengine wao hawakuafiki maelezo yaliyotolewa. Pakazuka upasi na chuki kubwa. Wale wasiokubaliana na Seikh walileta uadui. Walioafikiana wakajiunga katika Jumuiyya ya Ahmadiyya. Japokuwa hawa walikuwa wachache, lakini yao yalikuwa na nguvu ajabu.

Ndugu wa Sheikh Swaleh walimsusa, hakuwa pamoja nao na lolote. Kulikuwapo na kundi lenye watu sabini hivi, hili lilikuwa kila wakati kazi zake ni kuvuruga shughuli zote anazofanya Sheikh Swaleh. Walidiriki wamtowe duniani mapema zaidi, lakini wao wameondoka mmoja baada ya mwingine hadi wote sabini kupotea. Baadhi yao Sheikh Swaleh mwenyewe aliwazika. Hadi Sheikh Swaleh anafariki wale sabini wote walikwisha fariki. Allah Hufanya Apendavyo.

Pamoja na uadui huo wote kutoka kwa ndugu zake, lakini mjomba wake alikuwa pamoja naye. Mzee Abdullah Marunda alijiunga na Ahmadiyya, yeye na Waahmadiyya wengine walikuwa tayari wakati wote kumsaidia Sheikh Swaleh. Mwisho tawi la Jumuiyya likawa na watu wengi na imara.

ANAREJEA RUFIJI.

Sheikh Swaleh Mbaruku baada ya kuanzisha tawi kule Njinjo Kilwa, alirejea Rufiji pamwe na watoto wake kuendeleza kwa kila alichokipanda kwa kupalilia. Jumuiyya ya Rufiji ilikuwa na nguvu ajabu. Waumini wake walikuwa watowaji wazuri wa michango. Wao mara tu baada ya kuvuna mavuno yao kila mmoja alitoa mchango wake.

HODI MOROGORO

Huyu ndiye Sheikh Swaleh Mbaruku Kapilima Mbashiri wa kujitolea. Ni mwaka 1962 sasa anafika Morogoro zamani ulikuwa chini ya Jimbo la Pwani. Wakati huo Morogoro ilikuwa na Wanajumuiyya watatu tu. Bwana Mtumwa Abdullah wa Mikese, Mzee Chamchuwa Millonge na Dr. Dar wa Morogoro Mjini. Kama kawaida yake, Sheikh Swaleh hakulaza damu, mara moja alianza kazi ya Tabligh. Njia aliyopitia ni ile ile ya hekima na busara. Tahamaki, wakapatikana maalwatani wawili. Hao alikuwa mzee Aliy Ramadhani na Ramadhani Abdullah. Kwa pamoja jeshi lenye silaha kali likaanzishwa na Morogoro ikawaka moto. Watu kila pembe ya mji wakawa wanazungumzia Ahmadiyya.

Idadi ya watu ilipoongezeka kujiunga katika Jumuiyya ya Ahmadiyya, wazo la kupata Msikiti likawa dhahiri. Nafasi ikapatikana pale ambapo sasa hivi Msikiti ulipo. Zamani pale palikuwa nje ya mji wenyewe wa Morogoro, lakini leo ni katikati. Alhamdulillahi. Kwa kuwa Mzee Chamchuwa alikuwa mjenzi wa majumba, basi alisimamia vizuri kabisa hadi Msikiti unapatikiana. Jumuiyya ikasimama na matawi machache nje ya Morogoro yakapatikana, kama vile Mtibwa na Mkuyuni.

ANAENDA DUTHUMI

Sheikh Swaleh Mbaruku Kapilima aliondoka Morogoro mjini akaelekea Duthumi. Akawa mkulima mzuri wa mazao mbalimbali lakini hakusahau hata kidogo shughuli yake ya ubashiri. Kila uchao na uchwao mahubiri yalikuwa yanafanyika kwa juhudi na maarifa. Kwa msaada wa Allah tawi la Jumuiyya Duthumi likafunguliwa baada ya watu kadhaa kujiunga katika Ahmadiyya.

MAKTABA NDOGO.

Sheikh Swaleh aliendelea kutoa darasa kila inapobidi. Nyumbani kwake kulikuwa Maktaba ndogo ambayo ilikuwa na baadhi ya vitabu kadhaa. Kufuatana na maagizo ya mwenyewe vitabu hivyo iwe mikononi mwa Jumuiyya.

MWISHO WA MAISHA YAKE.

Sheikh Swaleh Mbaruku Kapilima ameuguwa muda mrefu kiasi. Siku moja alitembelewa na Mwalimu Abdul Imran kumjulia hali. Baada ya mazungumzo yao, Mwalimu Abdul Imrani alimwambia Sheikh Swaleh; "Sheikh nimeota kwenye ndoto nimekutana nawe na nikakuuliza mbona hauonekani bwana?" ulinijibu; "Mimi siku hizi nimehamia Makatul Mukaram". Baada ya siku mbili kupita, Sheikh Swaleh Mbaruku Kapilima Lihomba aliaga dunia. Ni kweli na ni hakika sisi ni wa Allah na kwake tutarejea.

Kwaheri; Allahu A'alam,

Safari ya Sialkot ya Seyidna Ahmad a.s. 1904

Kutoka uk. 7

Hudhura.s., Kwa hiyo tarehe 2 Novemba yaani siku hotuba watu wengi walifanya baiati juu ya mkono wa Hudhur as.

Baiati ya Hadhrat Chaudhari Nasrullah Khan:

Mheshimiwa Chaudhari Asadullah Khan Barrister, Amiri wa Jumuiya ya Waahmadiyya ya Lahore anasema kwamba baba yetu (Chaudhari Nasrullah Khan) pia alifanya baiati tarehe 2 au 3 Novemba tu na mama yetu alitangulia siku chache kufanya baiati kulingana na ndoto yake. Baba alikuwa mtu wa kutazama mambo kwa makini sana na alijua vizuri hali za Hudhur as. Katika kesi ya Sheikh Karmuddin Hudhur a.s. alimwita baba pia kama shahidi. Na kabla ya ushahidi alisema kwamba Bwana Chaudhari, katika ushahidi wako useme ile tu unayojua, kwayo baba aliathirika sana. Ukweli wa Jumuiya alijua hivi kwamba katika Sialkot Cantt ulikuwepo msikiti, imamu na msimamizi wake alikuwa Hadhrat Maulawii Abu Yusuf Mubarak Ali. Kwa vile alikuwa Mwahmadiyya, kwa hiyo msikiti pia ulikuwa chini ya usimamizi wa Waahmadiyya. Baada muda fulani wasiokuwa Waahmadiyya walitaka kunyang'anya msikiti huo. Hudhur a.s. alipoambiwa alisema kwamba kama Chaudhari Nasrullah Khan akikubali basi mfanyeni wakili katika kesi yenu. Kwa kufuatilia kesi barabara ilikuwa lazima kwamba asome vitabu vya Hudhur as. Basi alifanya hivyo. Alipohudhuria mahakamani aliona kwamba kwa kupinga Waahmadiyya masheikh wakubwa wakubwa wanakuja na wanasema uongo bila kusita lakini kila shahidi Mwahmadiyya anasema jambo lile tu analojua kwa yakini na kuchukia sana kusema uongo. Baba alichunguza kwa makini sana mwenendo wa Waahmadiyya na wasiokuwa Waahmadiyya na aliathirika sana na ushahidi wa Waahmadiyya. Wakati fulani hakimu alipomwuliza kwamba Bwana Chaudhari, je, u pia Mwahmadiyya? Hapo baba alisema kwamba sikuwa Mwahmadiyya lakini sasa inaonekana nitalazimika kuwa Mwahmadiyya na kwa kuithibitisha alieleza matukio ya kesi. Na kasema kwamba mtu ambaye wafuasi wake wanayo hali hii kwamba hawana cheo chochote cha dini lakini hata kuona hasara yao wazi wazi hawakosi kusema ukweli, basi mtu yule mwenye wafuasi wa aina hii hali yake itakuwaje. Nilikuwa nikisema kwamba siku ile watu wengi walifanya baiati. Baada ya baiati Hudhur a.s. alitoa hotuba ya nasaha ambamo alieleza makusudio ya baiati.

Sialkot ulikuwa mji ule ambamo aliishi kikazi kwa miaka minne kuanzia 1864 hadi 1868. Lakini katika zama zile watu wachache tu walijuana naye na watu wengine hawakujua hata jina lake. Sasa Hudhur a.s. alipoenda, alikuwa Mjumbe Adhimu wa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo kabla ya kuja kwake watu walijumuika kama vile kwa kupiga baragumu watu wanajumuishwa kwa amri. Na kwa kuona nadhara hiyo nadhara ya Jehlum ikaja mbele ya macho.

Kurudi Qadian – 3 Novemba 1904:

Tarehe 3 Novemba 1904 alitoka kwa kurudi Qadian. Nje ya makazini ya Hudhur a.s. kama kawaida watu walianza kujumuika tangu asubuhi. Kwa kutahadhari Hudhur alituma mapema akinamama stesheni kwa Hadhrat Mir Nasir Nawab. Jamaat ya Sialkot waliwalisha wageni chakula kabla ya saa nne asubuhi. Karibu saa sita Hudhur a.s. alishuka kutoka ghorofani. Halaiki kubwa ilijumuika. Ingawa mpango wa polisi ulikuwa imara sana hata hivyo baadhi ya wakati hao pia walishindwa. Kwa gari la Hudhur a.s. njia ilipatikana kwa taabu sana. Hudhur a.s. alipofika kwenye stesheni hapo pia kotekote palijaa. Kwa Hudhur a.s. behewa moja la daraja ya pili ilipangwa. Hudhur a.s. na ahli zake alipanda behewa ile. Gari lilipotoka, jukwaa ilijaa kwa sauti ya Assalamu alaikum na kwa heri.

Katika stesheni hiyo ilitokea kwamba gari lilipotoka jukwaa ndipo baadhi ya wapinzani wakawa uchi kwenye stesheni lakini hatuoni hapa umuhimu wake kueleza. Lakini kitendo hicho kilikuwa kinyume cha Islam bali kinyume cha ubinadamu kiasi hiki kwamba hata gazeti pingaji kali la Jumuiya Ahmadiyya "Ahle Hadithi" pia lililazimika kulalamika.

Stesheni ya Wazirabad:

Gari lilipofika Wazirabad, kwenye jukwaa la garimoshi hapo msongamano ulikuwa mkubwa zaidi kuliko awali. Hadhrat Hafidh Maulawii Ghulam Rasul Wazirabadi, kama awali, aliwahudumia ndugu zake kwa sharbati ya limau na soda. *Mungu Ampatie ujira bora.*

Kwenye stesheni ya Wazirabad garini pia watu wengi walifanya baiati. Wakati wa kurudi katika Lahore Daktari Seyid Muhammad Husain Shah aliwahudumia Hudhur a.s. na wenzake kwa chakula cha jioni. Usiku Hudhur a.s. alikaa Batala, asubuhi Jumuiya ya Batala ilileta chai na chakula. Hatimae karibu saa sita mchana, Hudhur a.s. kwa ahli na mahadimu zake alifika Qadian. *Alhamdulillahi alaa dhalika.*

Usalama Barabarani na Mazoea Yetu!

Na Abdillah Omary Kombo
Dar es Salaam



Ofisa polisi wa Usalama Barabarani akiwafundisha wanafunzi wa shule ya Msingi jinsi ya kuvuka barabara kwa kutumia alama za barabarani

Swala la matumizi sahihi ya barabara ni moja ya mambo muhimu katika jamii yeyote ile duniani. Vyombo vya usafiri vinavyotumia barabara vina faida kubwa na muhimu kwa matumizi yetu ya kila siku, lakini vikitumika vibaya bila kuzingazitia utaratibu vinaweza kuleta madhara makubwa ya uharibifu wa mali na hata kupoteza maisha ya watu. Ni Kwa maana hii ndio maana kumekuwa na juhudu mbalimbali katika ngazi zote kuanzia ngazi za chini kabisa za kijamaii mpaka za juu kabisa za kidunia. Mwaka huu Jumuiya ya kimataifa imeadhimisha kwa mara ya nne wiki ya usalama barabarani (8–14 May) iliyokuwa na kauli mbiu "Linda Maisha, Nenda Pole Pole" hii yote ni katika kuona umuhimu wa usalama barabanani sio tu wa vyombo vyenyewe vya usafiri bali na kwa watumiaji kuwa makini katika kufuata sheria zilizowekwa za usalama barabarani popote walipo.

Wahusika wa maswala haya wamekuwa wakitoa elimu maalum kwa watumiaji wa vyombo hivi na matumizi sahihi ya barabara ili kuondoa kama si kupunguza kadiri inavyowezekana ajali za barabarani. Juhudi hizi za utoaji wa elimu zimejigawa katika mazingira mbalimbali kutegemeana na wadau husika, wakishirikiana na wataalam wa idara na sekta mbalimbali za kijamii na za kiserikali.

Wapo wadau wakuu wa maswala ya usalama barabarani ambao nao hutumia muda na gharama kubwa katika kuhakikisha wanafadhili mafunzo ya matumizi sahihi za barabara, kwa madereva wa vyombo vya moto, waenda kwa miguu, ikiwa ni pamoja na kuweka alama sahihi za barabarani, nk wakishrikiana na idara husika za usalama barabarani vitengo kwa kuelimisha umma.

Moja ya Wadau hawa wakuu ni shirika linalojihusisha na michezo ya mashindano ya vyombo vya moto kama vile magari nk "Motor Sports" na maswala ya usalama barabarani lijulikanalo kama Automobile Association of Tanzania "AAT" Shirika hili mbali ya kuandaa mashindano ya magari lakini pia limekuwa likifanya kazi kubwa katika kuhakikisha wananchi wanakuwa na elimu ya kutosha ya matumizi sahihi ya vyombo vya moto wanapokuwa barabarani, na watumiaji wa kawaida wa barabara. Shirika hili limekuwa likifanya kazi kwa ukaribu sana na kitengo cha kutoa elimu kwa umma kutoka makao makuu ya usalama barabarani hapa nchini. AAT imeandaa mafunzo mengi kama nilivyosema hapo awali, miongoni mwa mafunzo hayo ni pamoja na kutoa mafunzo kwa waendesha bodaboda zaidi ya 1000 nchini ili kujua matumizi sahihi ya pikipiki zao wanapokuwa barabarani, matumizi ya kofia ngumu "Helment" kuheshimu alama za barabarani ikiwemo alama za Pundamilia {Zebra Cross} Taa za kuongozea magari barabarani {kwa miji yenye taa hizo} na mambo mengine mengi. Ingawa mafunzo haya yalifanyika jijini Dar es salaam lakini mipango inaendelea kufanywa ili mafunzo ya aina hii yaweze kufanywa katika miji mingine nchini.

Huenda mtu asione umuhimu wa maswala haya, kwani si kila siku watu wanatumia barabara kutoka sehemu moja kwenda nyengine, kwa miguu au kwa kutumia vyombo vya usafiri kama ilivyo mazoea kwa wengi, lakini kiukweli maswala ya usalama barabarani ni muhimu kuyajua na kuyafuata. Kujikumbusha mara kwa mara ni muhimu pia na kuondoa dhana kuwa wewe ni mkongwe wa kuendesha na kutumia barabara.

Inasemekana kuwa ajali nyingi husababishwa na makosa kabisa ya kutofuata sheria au alama za barabarani na kujiamini kupita kiasi. Mwendo ukibeba dhana nzima ya ajali zisizokuwa na sababu ya msingi. Hivyo kuwa na elimu na kuitumia elimu hiyo ni jambo la muhimu sana, hapa namaanisha, kuwa na elimu ni jambo moja, lakini kuelimika nalo ni jambo jengine, hapa mimi nasisitiza tuache kutumia barabara kwa mazoea, bali tufuate sheria za usalama barabarani.

Tuelimike na tutumie elimu sahihi tuliyopewa au tuliyofundishwa kwa vitendo na tuachane na maswala ya mazoea. Nakumbuka nilipokuwa mtoto nilikuwa nikiambiwa "vuka barabara mbio" lakini sikuwa nikiambiwa kuangalia kulia na kushoto kabla sijavuka, kitu ambacho ni hatari sana, maana unaweza kuingia barabarani mbio bila kuangalia pembeni na huenda gari liko karibu ukapata ajali.

Wakati najifunza kuendesha gari niliambiwa na mkufunzi wangu kuwa katika alama zote za kuongozea magari alama iliyo sahihi na wazi ni moja tu. Je unaweza kufikiria ni ipi? Taa Nyekundu, kwa maana ya kusimama, haina mjadala, ni kusimama tu. Nyengine zote lazima zifuatwe na neno kama ni salama. Iwe kijani ama rangi ya chungwa, lazima uangalie kama ni salama ndio kitendo kifuate.

Ingawa takwimu zinaonyesha kupungua kwa kiasi Fulani kwa ajali za barabarani hapa nchini lakini hali bado si ya kujivunia sana. Takwimu zinaonyesha bado kuna ajali nyingi tu za barabani hapa nchini. Kwa watoto nao wamekuwa wahanga wakubwa wa ajali za barabarani, hasa wanapokuwa wakitembea kutoka sehemu A kwenda sehemu B, Inasemekana umri wa watoto hasa kuanzia miaka 5 mpaka miaka 12 kuwa ni wa hatari kubwa zaidi ya kiusalama wakiwa barabarani. Wazazi tunashauriwa sana kuwa makini na watoto wenye umri huo, tunapowatuma au wanapokuwa wanatumia babaraba au unapokuwa nao barabarani.

Ni kwa maana hii shirika la AAT likaamua kuandaa mafunzo kwa waalimu na wanafunzi wa shule za awali, msingi, secondary na hata vyuo vya elimu ya juu kuhusu matumizi sahihi ya barabara.

Jumla ya shule 51 zilishirikishwa katika mradi huu mkubwa, ambapo walimu takriban 1000 nao walipatiwa mafunzo haya, kwa nadharia na kwa vitendo, ikiwa ni pamoja na vyuo vikuu viwili vya walimu, Dar es salaam College of Education "DUCE" na Al Haramain Islamic Teachers College. Waandaaji wa wafunzo haya AAT chini ya mratibu mkuu, Yusuf Ghor anaamini kuwa elimu hii inaweza kwa kiasi kikubwa kusaidia watoto kujua matumizi sahihi za barabara, Si hilo tu bali hata majumbani walimu hawa kama wazazi wanaweza kuwa mabalozi wazuri wa kutoa elimu hii katika nyumba wanazoishi.

Akimkaribisha mgeni rasmi katika hafla ya kutunuku vyeti kwa walimu na wanafunzi walioshiriki katika mafunzo hayo, Rais wa AAT Nizar Jivan alisema kuwa wakati umefika sasa kwa serikali kupitia wizara ya elimu, kuanzisha mitaala mashuleni ya masomo ya usalama barabarani kwa wanafunzi. Na kuwa hiyo inaweza kuwa chachu nzuri kwa wanafunzi kujifunza na kujua matumizi sahihi ya barabara.

Kamanda mkuu wa kikosi cha usalama barabarani nchini DCP Mohamed Mpinga alisema kuwa swala la usalama barabarani ni nyeti na kila mtu kwa nafasi yake anatakiwa kuchukua tahadhari, kwani sote tunataka kuishi na hatutaki kufa kwa ajali za barabarani, kama ambavyo kauli mbiu inavyosema "Hatutaki Ajali Tunataka Kuishi Salama" Pia kamanda Mpinga alisema kuna haja sasa ya kuanzisha vilabu vya kujifunza mambo ya usalama barabarani mashuleni kama ilivyo kwa vilabu vya masomo mengine. Alisema kwa njia hii, kupitia vilabu hivi, wanafunzi wataweza kujifunza maswala mbalimbali ya matumizi sahihi na sheria za usalama barabarani. Hii itasaidia wanafunzi kuwa na umahiri mkubwa wa matumizi sahihi ya barabara. Na hivyo kupunguza kama si kuondoa kabisa tatizo hili sugu katika nchi nyingi duniani, tatizo ambalo kila uchau linagharim uharibifu mkubwa wa mali, maisha ya watu nk. Tunaamini wadau, wenye dhamana za kimadaraka na jamii kwa ujumla, sote kwa pamoja tukiamua kwa dhati ya nafsi zetu, kwa hakina tunaweza kufanya mabadiliko makubwa katika swala zima la usalama barabarani. Naamini Ajali Ina Kinga Iwapo Sote Tutaamua Kwa Dhato Kijikinga. Mengine Tumuachie Mwenyezi Mungu Mwenyewe.

Maadhimisho ya siku ya Ukhalifa - 2017

Kutoka uk. 12

Tanzania.

Maadhmisho hayo yalifanyika siku ya Jumapili tarehe 28/5/2017 ambapo Wanajamaat wapatao 500 kutoka matawi yote ya mkoa wa Dar es Salaam walihudhuria.

Maadhimisho hayo yalifunguliwa kwa usomaji wa Quran tukufu iliyosomwa na Mwl Hassan Mwalimu na kufuatiwa na shairi la Karne ya Ukhalifa shani ya Ahmadiyya lililoimbwa na Bw. Jalaluddin Malik Mbawala.

Akifungua maadhimisho hayo Naib Amir Jamaat Ahmadiyya nchini Bw. Issa Mwakitalima aliwakumbusha wajumbe juu ya msingi mzima wa uwepo wa Maadhimisho hayo na kwamba kuna haja ya kusikiliza kwa makini hotuba zitakazotolewa ili kuweza kufaidika na maadhimisho hayo.

Baadae zilifuata hotuba kadhaa zilizotolewa na Masheikh na Walimu wa Jamaat. Miongoni mwa waliotoa hotuba katika maadhimisho hayo ni Mwl. Abdallah Mbanga, Bw. Ali Khamis Mbambwa (Sadr sahib Ansarullah) na sheikh Ame sahib. Katika hotuba hizo zote kimsingi wazungumzaji walivyowakumbusha wasikilizaji juu ya Historia ya Ukhalifa baada ya Mtukufu Mtume s.a.w. pamoja na ahadi ya Mwenyezi Mungu ya kuleta tena Ukhalifa kwa wale watakaomuamini Yeye na Mtume wake s.a.w. ki ukweli baada ya Ukhalifa huo kutoweka duniani.

Aidha wazungumzaji walielezea juu ya baraka za Ukhalifa na maendeleo ya Jamaat sambamba na uwepo wa Ukhalifa ikiwa ni moja ya ushahidi wa ukweli wa Jamaat Ahmadiyya.

Haja ya kuwa watiifu na kushika nidhamu ya Ukhalifa ni miongoni mwa mada iliyotolewa kwenye maadhimisho hayo ambapo wasikilizaji walikumbushwa juu ya ulazima wa kushika utii na kujenga ukaribu na Hadhrat Khalifatul Masih kwa kumuandikia barua lakini zaidi kwa kutekeleza maagizo na miongozo anayotupatia mara kwa mara, ikiwemo kufuata nidhamu yote ya ukhalifa.

Akifunga maadhimisho hayo, Amir sahib Jamaat Ahmadiyya Tanzania Maulana Tahir Mahmood Chaudhry aliwakumbusha Wanajumuiya juu ya msingi wa maadhimisho hayo na yaliyo kama hayo kwamba hayafanyiki kama zifanyikavyo sherehe za kidunia; bali lengo la maadhimisho hayo ni kutukumbusha umuhimu wa kihistoria wa matukuo hayo sambamba na utekelezaji wa majukumu yetu katika kuenzi neema za Allah ili tuweze kufaidika nazo.

Kimakhsusi Amir sahib aliutaja Ukhalifa kuwa ndio neema kubwa leo kwa Waislamu na kusema kuwa maendeleo yote ya Jamaat yanapatikana kwa sababu ya baraka za kuwa kwetu na Ukhalifa tu.

Hivyo aliwaomba Wanajamaat wote nchini kujenga ukaribu maalum na Ukhalifa ambapo njia moja iliyo na athari kubwa leo ni kusikiliza hotuba za Ijumaa na zinginezo za Hadhrat Khalifatul Masih kupitia MTA.

Kusikiliza MTA alisema, ni njia moja nzuri sana ya malezi ya familia zetu na hasa watoto wetu ambao wanazungukwa na mazingira mengi hatarishi kwa ajili ya malezi yao ya kimaadili na kiroho.

Hivyo Amir sahib aliwaomba wanajamaat wote walio na uwezo na ambao hawajaweka mawasiliano ya MTA majumbani mwao wafanye hivyo haraka iwezekanavyo na akamtaka kila rais wa tawi kuweka ushawishi na uangalizi maalum kwa watu wa tawi lake.

Aidha Amir sahib aliwaomba wanajumuiya kwamba baada ya kuwa na MTA majumbani mwao wahakikishe wanasikiliza matangazo yake badala ya kusikiliza idhaa zingine na akatangaza rasmi kwamba kuanzia sasa vifaa vyote vya MTA vili

vyowekwa kwa gharama za Jumuiya havitoruhusiwa kutumika kwa ajili ya kuangalia idhaa za televisheni zingine.

Baada ya kufungwa kikao kwa maombi na kufutiwa na sala ya Adhuhuri na Alasiri washiriki wote walipata chakula cha pamoja kabla ya kutawanyika na kurudi majumbani kwao.



Sehemu ya washiriki kwenye maadhimisho ya siku ya Ukhalifa yaliyofanyika Kitonga Dar es Salaam tarehe 28/5/2917, wakifuatilia hotuba zilizokuwa zikitolewa katika maadhimisho hayo.

Kuwatendea wanawake kwa wema ndicho kipimo cha ubora wa wanaume

Kutoka uk. 12

Hivyo, ikiwa wanaume wengi wanataka kuzingatia mifano hii, wajitathmini juu ya tabia zao mbalimbali wanapokuwa nyumbani. Ikumbukeni hadithi hii "Mbora wa vitendo na khulka miongoni mwenu ni yule anayewatendea wake zake kwa wema". Hivyo, kuwatendea wake kwa wema ni alama kubwa ya mtu kuonyesha kiwango chake cha Imani.

Kuhusiana na wajibu wa mume na kuwatendea wema wake, Masih Aliyeahidiwa (a.s) alisema, "Isipokuwa upujufu tu, lakini madhaifu yote, na tabia nyingine za kuchukiza za mwanamke zinatakiwa zivumiliwe. Ni aibu kubwa kwa mwanaume kumpiga mwanamke…" Masih Aliyeahidiwa (a.s) aliwahi kusema kwamba: Wanajamat wetu hawatakiwi kuwa wakali na wenye hasira dhidi ya wake zao. Masih Aliyeahidiwa (a.s) pia alisema, "Kama inawahi kutokea nikanyanyua sauti yangu dhidi ya mke wangu, basi ninajaribu kujizuia kutamka maneno makali na ya kumuumiza. Pia ninafanya Istighfar kwa wingi (kuomba msamaa kwa Allah) na ninasali sala za nafal kwa bidii kubwa na kutoa sadaka…"

Hivyo, wale ambao sio wema kwa wake zao, imani zao zimo hatarini. Ni lazima wajiangalie sana kwani mtu ambaye hayuko katika viwango vya juu kabisa vya kiimani, anaweza kuporomoka wakati wowote. Akiwaasa watu wa aina hiyo, Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema, "Kama mtu sio mcha Mungu, inawezekanaje sasa mke wake awe mchaMungu? Masihi Aliyeahidiwa (as) zaidi anasema, "Hakika, kama mtu anakuwa mchaMungu, mke anaweza pia kuwa mchaMungu".

Hapa nimeona kuwa wanawake wanafuata dini zaidi. Wanalalamika baadhi ya wakati kwamba waume zetu hawaelekei kwenye dini. Hawasali, wanatizama vipindi kwenye TV visivyofaa na visivyo na maadili na wanapuuza majukumu yao ya kuwalea watoto. Pia wanawakaripia na kuwapiga watoto. Katika nchi hizi, mambo ya aina hiyo huwa yanapelekwa polisi na yanaleta jina baya kwa Jumuiya yetu. Zaidi ya hayo, watu wa aina hiyo wanapata adhabu za kidunia pia ikiwa ni ghadhabu ya Allah Mwenyezi.

Hivyo, kama mnapenda kuwa na nyumba zenye amani, kama mnataka kuviimarisha vizazi vijavyo na kuwadumisha katika dini, basi wanaume wanapaswa kuwa waangalifu wa hali zao. Hivyo, hiki ndicho kiwango. Jitihada zenu zote za mahubiri na za kupata elimu ya dini ni za bure, kama sio wazuri kwa familia zenu. Wanaume wasipochukua majukumu yao kwa umakini, nyumba zinavunjika na maisha ya watoto yanateketea. Wanaume wasilazimishe hijabu kwa wanawake kwa kutumia nguvu lakini wanawake nao ni lazima wajue kwamba wanahitajika kufunika vichwa vyao na miili yao sawa na mahitajio ya staha. Hili ni Agizo la Allah Mwenyezi kwa hiyo ni lazima waliangalie hilo. Masihi Aliyeahidiwa (as), akielezea hili, anasema, "Uhusiano kati ya mume na mke ni lazima uwe kama ule wa watu wawili wenye urafiki wa kweli na wa dhati… kama uhusiano wa mtu na mkewe sio mzuri, anawezaje kuwa na amani na Mungu? Mtume Mtukufu (saw) anesema, "Mbora wenu ni yule ambaye ni mbora kwa mkewe.

Zaidi ya hayo, wanaume wanahitaji kuelewa majukumu yao kama baba. Mababa ni lazima watekeleze majukumu yao ya kuwafunza na kuwalea watoto. Bilkhusus, wakati wavulana wanafikia umri wa miaka saba au nane, wanakuwa wanahitaji uangalizi wa baba zao. Wanaume na kina baba ni lazima waonyeshe mifano yao mizuri. Pale kina baba wakionyesha heshima na kujali watoto wao, wanakuwa na tabia nzuri. Uhusiano mzuri wa baba na watoto wake unawafanya wajisikie salama. Hivyo, kuingiza ndani ya watoto hisia za usalama, ni lazima kwamba kina baba watumie muda fulani katika kazi za kimapumziko na watoto wao na wawaombee. Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema, "Ninawaombea watoto wangu na ninawataka wawe na mtazamo mpana wa kufuata sharia za khulka njema (mafundisho yetu ni nini, sharia zake ni zipi, kanuni zake ni zipi, tunawaangalia) na si zaidi ya hapo. Zaidi ya hapo ninamtegemea Allah Mwenyezi kikamilifu kwa uhakika ambao mbegu ya bahati njema inarithika kwa kila mmoja wao itatoa maua katika wakati wake maalum. Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema zaidi, 'Kuweni kwa namna ambayo ni mfano bora kabisa kwa watoto wenu na kwa hili ni lazima kwamba mtu ajirekebishe binafsi yake.

Islamu pia inasisitiza kwamba 'nyie (watoto) pia mna majukumu. Mnapofikia baleghe, mnakuwa na majukumu fulani kwa wazazi wenu ambayo ni lazima myatekeleze. Wakati fulani Mtume Mtukufu (saw) alimuambia sahaba aliyetaka kwenda kwenye Jihad kwamba kama wazazi wako wapo hai, ni lazima uwahudumie, hiyo ni Jihad kwako". Hivyo, mtu anaweza kupima umuhimu wa kuwahudumia wazazi wake kutokana na hili. Hazrat Abu Saeed Al-Siyaadi (ra) anasimulia "Tulikuwa tumekaa pamoja na Mtume Mtukufu (saw) wakati mtu mmoja kutoka Bani Salama alipotokea na kuuliza 'Ee Mjumbe wa Allah! Kuna jambo lolote jema ninaloweza kulifanya baada tya wazazi wangu kufariki?' Mtume Mtukufu (saw) akasema: Naam! Uwafanyie maombi na kuwatakie msamaha. Utekeleze zile ahadi walizozifanya kwa watu. Uonyeshe wema na huruma kwa ndugu zao wote na marafiki zao. Kisha katika tukio jingine Mtume Mtukufu (saw) alisema: "Yeyote anayetaka kuishi maisha marefu na kwamba pato lake libarikiwe basi aonyeshe wema na huruma kwa wazazi wake na aonyeshe heshima kwa ndugu zao."

Hivyo, watoto sio wawe wanaomba tu toka kwa wazazi wao, bali, wanapofikia baleghe wanakuwa na majukumu fulani na haki ambazo wanapaswa kuwatendea wazazi wao. Na hasa baada ya ndoa, mtu awe makini zaidi na majukumu haya. Kama mtu anatumia busara na kutimiza haki za mke wake na pia za wazazi wake, kama mtu anakuwa na heshima kwa mama na baba mkwe basi kunakuwa kamwe hakuna migogoro yoyote kwenye nyumba, ambayo aina yake huwa inaonekana.

Kwa vyovyote vile, mwanamume ni lazima atimize majukumu mbalimbali yaliyowekwa kwake. Daima aonyeshe mfano nyumbani ambao kwao unaleta hali ya upendo na huba. Mwanamume ni mume, na pia ni baba na ni mtoto. Kwa hiyo, mtu ni lazima aelewe majukumu yake sawa na hali zake mbalimbali.

Ninamuomba Allah Amuwezeshe kila mmoja kupata hili. Amin.

MAFUNZO KWA VITENDO



Baadhi ya Atfaalul Ahmadiyya wakifanya maonyesho ya vitendo ya jinsi ya kushona Sanda ya Mwanamume wakati wa mashindano ya usomaji na uhifadhi wa Qurani tukufu yaliyofanyika ndani ya mwezi mtukufu wa Ramadhani, Makao makuu Dar es Salaam

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Shab./Ramadh. 1438 AH | MEI/JUNI 2017 | Hijrat/Ihsan 1396 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Ayoub bin Musa r.a. kutoka kwa baba yake kisha kwa babu yake ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Hakuna baba aliyempa mwanawe zawadi bora kuliko adabu njema, yaani ulezi bora. (*Tirmidh*)

Kuwatendea wanawake kwa wema ndio kipimo cha ubora wa wanaume - Khalifa mtukufu

Na Mwandishi Wetu

Baada ya *Tashahhud, Taa'udh* na *Surat Fatihah* Hadhrat Amir-ul Muminin (atba) alisema:

Mafundisho ya Islam yaliyofunuliwa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w), yanatupatia muongozo katika kila jambo. Ikiwa kila mmoja wetu atekeleze mafundisho haya, jamii nzuri itatengenezwa. Kuna amri zisizohesabika katika Quran tukufu, ingawaje Allah Mtukufu amesema:

"Bila shaka mnao mfano mwema kwa Mtume wa Allah"... (33:22)

Hivyo mafanikio ya kweli yatapatikana ikiwa tutaiweka mbele mifano hii kwa kila jambo kubwa na dogo.

Kwa muktadha huu, nitasema jambo fulani kuhusu majukumu ya wanaume katika nyanja mbalimbali. Mwanaume ana jukumu kama mlinzi wa familia na pia kama mume. Ana jukumu kama baba lakini pia kama mtoto. Ikiwa kila mwanaume atambue majukumu haya na ajaribu kuyatimiza, itakuwa ni njia ya kujenga amani katika jamii na kusimamisha mapenzi na mapatano.

Baadhi ya wanaume, wanafikiria kwamba wana mamlaka yasiyo na mipaka kama viongozi wa familia, wanajiingiza katika magomvi ya nyumbani na wanafanya dhulma kwa watoto. Hivyo, ikiwa mtu anataka kumtendea mke wake na watoto wake kama watu wajinga, basi haina haja ya yeye kufanya Baiati ya Masih Aliyeahidiwa (a.s). Mtukufu Mtume (s.a.w) akiwa kama mlezi wa familia, aliifanya familia yake kuwa kipaumbele cha kwanza katika kukubali, umuhimu wa kusimamisha tauhidi (umoja wa Mwenyezi Mungu). Ingawa, alifanya hivyo kwa mapenzi na hurama na sio kwa kutumia nguvu.

Vilevile Hadhrat Aisha (r.a) anasimulia kwamba, Mtume Mtukufu (s.a.w) alipokuwa anaamka usiku kwa ajili ya sala za nafal alikuwa anatuamsha kwa kutunyunyuzia maji usoni, ili tusali sala za nafal na tutimize wajibu wetu mbele ya Allah. Pia, Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa akisaidia kazi, ambazo zilikuwa ni majukumu ya wake zake. Hadhrat Aisha (r.a) anasimulia kwamba alikuwa anashona nguo zake, anatengeneza viatu vyake na anarekebisha vifaa vya nyumbani kama vile ndoo za maji n.k.

Endelea uk. 11

Maadhimisho ya siku ya Ukhalifa - 2017

Amir sahib Afungua Msikiti Mpya Kitonga

Apiga marufuku vifaa vya MTA vya Jamaat kutumika visivyo

Na Mwandishi Wetu

Kwa mara nyingine Jamaat ya Mkoa wa Dar es Salaam imefanya maadhimisho ya siku ya Ukhalifa katika kuendeleza kumbukizi la kuhuisha tena kwa neema ya Ukhalifa katika umma wa Mtukufu Mtume s.a.w. kupitia ujio wa Masihi aliyeahdiwa a.s. kama ilivyotabiriwa.

Maadhimisho hayo yalifanyika kwenye viwanja vya Jamaat vilivyopo Kitonga, kata ya Msongola, nje kidogo ya jiji la dar es Salaam.

Ingawaje maadhimisho haya ya Dar es salaam ni ya kimkoa lakini huchukua sura ya kitaifa utokana na uwepo wa Amir Jamaat

Endelea uk. 10



Amir na Mbashiri Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry aliyeketi mbele (katikati) akisikiliza kwa makini hotuba iliyotolewa na Sheikh Ame sahib katika maadhimisho ya siku ya Ukhalifa yaliyofanyika Kitonga Dar es Salaam tarehe 28/5/2917.